

jarida la

# WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU | [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz) | Juni 23, 2021



## Mwaka wa Vipaji



Wizara HabariTz




Wizara\_habaritz



Wizara\_HabariTZ

# Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo



# TAHARIRI

## SERIKALI KUBORESHA MAZINGIRA YA SANAA NA MICHEZO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katikati ya mwezi Juni 2021 akiwa Jijini Mwanza akizungumza na vijana alisema kuanzia mwezi Desemba mwaka huu wasanii wataanza kulipwa Mirabaha yao kupitia kazi za Sanaa zinazochezwa katika redio, runinga na mitandao ya kijamii.

Kauli hiyo ya Mhe. Rais na Serikali imekuwa jibu la kilio cha wasani kwa muda mrefu, huku maamuzi hayo ya Serikali yamekuja wakati ambapo sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo zinaajiri vijana wengi.

“Tumeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ili kusaidia timu zetu za Taifa, tumefuta kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika nyasi bandia. Hivyo, majiji na Manispaa changamkieni fursa hii kupata viwanja bora”. Pia Mheshimiwa Rais alilipigia chapuo suala hili.

Aidha, Mhe. Rais alitoa wito kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutumia fursa hiyo kuboresha viwanja ambavyo inavimiliki katika mikoa na majiji yote nchini ili kuweka mazingira sahihi ya kuendesha michezo nchini.

Sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tunayachukulia maagizo ya Mhe. Rais aliyoyatoa kwa Wizara akiwa Jijini Mwanza kwa uzito wake kuanzisha vituo vya michezo (Sports Academy) kila Mkoa ili kukuza vipaji na Sekta ya Michezo hapa nchini.

Tunaamini maagizo haya yamekuja wakati sahihi kwa mfano suala la mrabaha lililokuwa kero kubwa kwa wasanii, ni vizuri wafanyabiashara, wadau wa wasanaa na jamii kwa ujumla tushirikiane kuhakikisha wasanii wanapata haki zao ili kuikuza sanaa ya kitanzania na kuibua fursa nyingi zaidi za ajira.

Kwa upande wa taasisi zinazomiliki viwanja vya michezo kama ilivyoagizwa na Mhe. Rais, wale wasio na uwezo wa kuboresha viwanja hivyo wawape fursa hiyo wenye uwezo wa kufanya hivyo huku kwa Upande wa Sport Academy, tayari suala hili limeshaingizwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Tunaimani kwa upande wetu sisi kama Wizara yenye dhamana ya sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tutatoa ushirikiano wote unaohitajika kuhakikisha kuwa shabaha ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kuboresha mazingira ya michezo, sanaa na utamaduni yanaboreshwa inatimia kwa kila mdau kutimiza wajibu wake ipasavyo.



## Wasanii kuanza kulipwa mirabaha mwezi Desemba, 2021

Na Shamimu Nyaki, **Dodoma**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema kuanzia mwezi Desemba mwaka huu wasanii wataanza kulipwa mirabaha yao kupitia kazi za Sanaa zinazochezwa katika redio, runinga na mitandao ya kijamii.

Mhe. Samia amesema hayo Juni 15, 2021 Jijini Mwanza alipokuwa anazungumza na vijana wa Mkoa huo kwa niaba ya vijana wote nchini, ambapo amesema Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo inajiri vijana wengi hivyo Serikali inendelea kuimarisha sekta hizo.


“Tumeanzia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ili kusaidia timu zetu za Taifa, tumefuta kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika nyasi bandia, hivyo majiji manispaa changamkieni fursa hii kupata viwanja bora” amesisitiza Mhe. Samia.

Aidha, Mhe. Rais ametoa wito kwa Chama cha Mapinduzi kutumia fursa hiyo kuboresha viwanja ambavyo inavimiliki katika mikoa na majiji yote nchini ili kuweka mazingira sahihi ya kuendesha michezo nchini.

Vilevile ameiagiza Wizara ya Habari

Utamaduni, Sanaa na Michezo kuanzisha vituo vya michezo (Sports Academy) kila Mkoa ili kukuza vipaji na sekta ya michezo hapa nchini.

Awali Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa ametoa wito kwa wafanyabiashara na watoa huduma kutumia wasanii katika kutangaza huduma na biashara zao kwa kuwa wasanii wana wafuasi na ushawishi mkubwa katika jamii, huku akisisitiza vijana ambao wanavipaji kuvi-onyesha ili viwapatie ajira.



## Tanzania yamlilia Kaunda

Adeladius Makwega, **DODOMA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametoa pole kwa Rais wa Zambia Edgar Lungu kutokana na msiba wa Rais wa Kwanza wa Taifa la hilo Keneth Kaunda.

“Nimesikitishwa na msiba huo wa Rais wa Kwanza wa Zambia Kenneth Kaunda, Mungu amlaze pahala pema peponi.” Taarifa hiyo imemnukuu Mhe. Rais Samia.

Tanzania inamkumbuka Kenneth Kaunda maarufu kama (KK) ambaye alikuwa Rais wa kwanza wa Zambia, mzalendo, mwanaharakati za Ukombozi wa Bara na mwana mwema wa Afrika aliyeipenda hatua iliyopelekea kuunga mkono

vuguvugu za ukombozi wa Bara zima la Afrika kwa kushirikiana kwa karibu na Rais wa Kwanza wa Tanzania Julius Nyerere pamoja na viongozi wengine wa Afrika wa wakati huo.

Miaka ya 1950, Kaunda alikuwa mtu muhimu katika vuguvugu la kupigania uhuru wa Rhodesia ya Kaskazini (sasa Zambia) kutoka kwa Uingereza.

Kifo chake ni pigo kwa taifa lake na Afrika kwa ujumla ambapo Vyombo vya Habari na wengine wakinukuu ukurasa wa facebook wa mtoto mkubwa wa Mzee Kaunda anayefahamika kama Kambarage ambaye anabainisha, “Nina huzuni kubwa

kuwa mzee amefariki dunia, ninawaomba tumuombee.”

Msiba huo umewagusa watu mbalimbali akiwamo nahodha wa zamani wa timu ya Taifa ya Zambia (K.K Eleven) Kalusha Bwalya aliyenusurika kifo katika ajali ya ndege iliyogharimu maisha ya watu 30 wakiwamo wachezaji 18 viongozi na makocha wa timu hiyo timu mwaka 1993 ambaye amewapa pole taifa lote la Zambia, familia ya Mzee Kaunda, Wazambia wote na Waafrika kwa ujumla na kuwaomba wawe na faraja katika kipindi hiki kigumu. Apumzike kwa amani.



## Somo la Elimu kwa Michezo kufundishwa kwa wanafunzi wote nehini

Na John Mapepele, Mtwara

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameelekeza somo la Elimu kwa Michezo lifundishwe kwa wanafunzi wote katika Shule za Msingi na Sekondari.

Waziri Mkuu ametoa maelekezo hayo Juni 08, 2021 Mkoani Mtwara alipofungua mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari (UMI-TASHUMTA na UMISSETA) ambapo amesema matarajio ya Serikali ni kuona wanafunzi wakionyesha uwezo na nidhamu ya hali ya juu ili kuleta mafanikio kwa taifa.

Amesema, Serikali inaendelea na jitihada za kuanzisha tahasusi za Michezo kwa wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6 ili kupata mafanikio katika sekta na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa viwanda.

“Nasisitiza Wizara husika kuangalia mitaala iliyopo kama inakidhi mahitaji ya sasa na kuchukua hatua stahiki pale ambapo kutaonekana kuna upungufu, nihimize kuboreshwa kwa vyuo vya ualimu ili viimarisha masomo ya Elimu kwa Michezo hatua itakayomuwezesha kila mhitimu kuwa na ujuzi wa ufundishaji wa michezo” amesisitiza Waziri Mkuu.

Pia Mhe. Majaliwa amesisitiza wito

wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan wa kuwahimiza wananchi kufanya mazoezi ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, huku akisisitiza kuendelea kuunda vikundi vya mazoezi ya ukakamavu (Jogging) na matamasha mbalimbali ya michezo pamoja na kujijengea utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara.



## Mhe. Majaliwa: Tufanye mazoezi tuimarisha Afya zetu

Na Shamimu Nyaki, **DODOMA**

Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa amewaa-sa watanzania kujijengea utaratibu wa kufanya mazoezi mara kwa mara ili kujiepusha na magonjwa pamoja na kuimarisha afya zao.

Waziri Mkuu ameyasema hayo, Juni 12, 2021 Jijini Dodoma alipozindua Bonanza la Michezo (Pamoja Bonanza) lilioandaliwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Bunge la Tanzania ambalo limehusisha mbio fupi, mazoezi ya viungo pamoja na michezo mbalimbali katika Uwanja wa Jamhuri Jijini hapo.

“Bonanza hili limeandaliwa kwa ajili

ya kutuhamasisha umuhimu wa kufanya mazoezi ili kuimarisha afya na hatimaye kuongeza ufanisi katika kazi zetu, pamoja na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ambayo wengi tumekua wahan-ga”amesema Mhe. Majaliwa.


Waziri Mkuu ameongeza kuwa, magonjwa hayo ambayo yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya vilevi, kutoshiriki mazoezi au kufanya shughuli za kutumia nguvu pamoja na kutozingatia lishe bora yamekua chanzo cha gharama kubwa za afya kwa Serikali na kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Aidha, Mhe. Majaliwa ametoa rai kwa watanzania kushiriki mazoezi, kuzingatia mlo sahihi kwakua kinga ni bora kuliko tiba ambapo pia amesisitiza kuundwa kwa vikundi vya mazoezi ya ukakamavu (Jogging) pamoja na kushiriki matamasha mbalimbali ya michezo.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akifanya mazoezi kwenye Bonanza la Michezo (Pamoja Bonanza) lilioandaliwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Bunge la Tanzania hivi karibuni.







## Serikali kuanzisha Kituo cha Michezo katika Chuo cha Michezo Malya

Na John Mapepele, **MTWARA**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa amesema Wizara inatarajia kuanzisha kituo maalum cha kuendeleza michezo katika Chuo Cha Maendeleo ya Michezo Malya ili kuendeleza vipaji vina- vyopatikana.

Waziri Bashungwa amesema hayo Juni 08, 2021 Mkoani Mtwara wakati wa ufunguzi wa mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari (UMI-TASHUMTA na UMISSETA) yaliyo- fanywa na Waziri Mkuu wa Tanza- nia Mhe. Kassim Majaliwa.

"Muamko na hamasa mnayoiona leo hii, ni ushirikiano wa Wizara ya

Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya mawaziri, makati- bu wakuu na wataalam" amesema Waziri Bashungwa.

Waziri Bashungwa amesema, matarajio ya Serikali ni kusimamia michezo vizuri katika ngazi ya chini ambayo itakuwa ni chimbuko kubwa la kuvuna vipaji ambavyo vitaendelezwa hatimaye kupata wachezaji wenye weledi, watakaoc- heza timu za Taifa, lakini pia watakaoc- heza michezo ya kulipwa, na kupatia ajira.

Katika mashindano hayo, vyama

vya Michezo vya Kitaifa, vilabu, watalaam wa kuvumbua vipaji (scouters) kutoka Taasisi ya Mbwana Samatta pamoja na wata- laam kutoka Sweden wamealikwa ili kupata fursa ya kuona vipaji katika mashindano hayo.

Katika ufunguzi huo, Naibu Waziri Ofisi Ya Rais TAMISEMI Mhe. David Silinde amesema malengo makuu ya mashindano hayo ni pamoja na kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kukuza vipaji vya michezo kwa kuibua na kujenga umoja wa kitaifa, mshikamano na upendo baina ya wanafunzi wangali katika umri mdogo ili kuimarisha taaluma ya michezo kwa wanafunzi na kuwajengea ujuzi na maarifa.



## Naibu Waziri Gekul: Wizara inagusa hisia za watu wengi

Na Shamimu Nyaki, Dodoma

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul amesema Sekta za Wizara hiyo zinagusa hisia na maisha ya watu wengi katika maisha ya kila siku.

Mhe. Gekul amesema hayo wakati anachangia na kujibu maswali ya Wabunge wakati wa kujadili hoja ya Waziri Mhe. Innocent Bashungwa alipowasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo hivi karibuni Bungeni Jijini Dodoma ambapo takriban Wabunge 25 wamechangia hotuba hiyo moja kwa moja na Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi.

“Hii ni Wizara inayogusa hisia za watu, huburudisha, elimisha na

kuunganisha watanzania. Kupitia michezo wananchi wanaimarisha afya zao na kupunguza bajeti ya dawa ambapo tayari Serikali kushirikiana na Wadau zipo shule za kulea vipaji vya michezo” amesema Mhe. Gekul.

Mhe. Gekul amesema Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambalo ndiyo waratibu wa michezo nchini mpaka sasa limesajili vyama vya michezo 12, vilabu 89, taasisi tano za kimichezo, wakuzaji vipaji vya michezo 11 vituo vya michezo vine na mawakala wamichezo 21.

Aidha, ameongeza kuwa marekebisho ya Katiba ya Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Vyama vya michezo vinne ambavyo ni Shirik-

isho la Mpira wa Miguu Tanzania, Shirikisho la Riadha Tanzania, Chama cha Michezo ya Jadi Tanzania na Chama cha Mpira wa Miguu cha Wilaya ya Mpanda vilipitiwa, kuboreshwa na kuidhinishwa na Msajili wa Vyama vya Michezo.127 ikiwa ni hatua ya kuimarisha michezo.

Ili kuboresha michezo nchini, Mhe. Gekul ameongeza kuwa Chuo cha Michezo Malya kimehuisha mitaala ya ufundishaji ambayo sasa inaendana na mahitaji ya soko la michezo ndani na nje ya nchi hatua ambayo itaongeza idadi ya michezo inayofundishwa ikiwemo mpira wa kengele kwa ajili ya watu wenye uoni hafifu, mpira wa meza na vinyoya.



# Tanzania Mwenyeji Mashindano ya Mchezo wa Kabaddi

Na Octavian Kimario, **DAR ES SALAAM**

Mashindano ya Afrika ya mchezo wa Kabaddi kwa mwaka 2021 yanatarajiwa kufanyika hapa nchini kuanza Juni 29 hadi 5 Julai, 2021 katika Ukumbi wa Ubungo Plaza Jijini Dar es salaam.

Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul Juni 21, 2021 ametembelea kambi ya timu ya taifa ya mchezo huo katika shule ya Sekondari Nguva wilayani Kigamboni Jijini Dar es Salaam, ambapo amewataka waratibu wa mchezo huo kutoa elimu ili jamii iutambue mchezo huo.

"Natoa rai kwenu kuzishirikisha sekta nyingine katika fursa hii muhimu, mfano sekta ya Utalii, wanaweza kutumia fursa iliyopo kutangaza vivutio vya Utalii vilivyopo nchini kwa mataifa ambayo yanakuja kushiriki mashindano haya," amesema Mhe. Gekul.

Aidha, Mhe. Gekul amewataka wachezaji waliopo kambini kufanya mazoezi kwa bidii ili kulibakisha kombe la mashindano hayo nyumbani, huku akipongeza wadhamini waliojitokeza kudhamini kambi hiyo na kutoa rai kwa wadhamini zaidi kujitokeza.

Mhe. Gekul ameongeza kuwa Serikali inaendelea kuipa kipaumbele michezo mbalimbali inayofanya vizuri ndani na nje kwakuwa inasaidia kutangaza nchi, kuibua vipaji pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana.

Mashindano hayo yanatarajiwa kushirikisha nchi sita Kenya, Mauritius, Misri, Cameroon Zimbabwe na wenyeji Tanzania ambapo wageni kutoka katika nchi zaidi ya 20 za Afrika wanatarajiwa kuwasili hapa nchini kwa ajili ya kuratibu na kushuhudia mashindano hayo.



# Wasanii wa kizazi kipya wafunika UMITASHUMTA, UMISSETA 2021

Na Joseph Kigingi, **MTWARA**

Wasanii wa muziki wa kizazi kipya, taarabu na singeli wamekuwa miongoni mwa kitutio kikubwa walipopanda kutoa burudani wakati ufunguzi na ufungaji wa Mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Sekondari (UMISSETA) kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara na kuyafanya mashindano ya mwaka huu kuwa na hamasa kubwa tofauti na mashindano yote ya awali.

Mashindano ya UMISHUMTA yaliyofunguliwa Juni 08, 2021 na Waziri Mkuu, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ambapo kundi la wasanii likiongozwa na Ibrah kutoka Konde Gang, Beka Flavour, Peter Msechu na Linah Sanga, msanii maarufu wa Singeli Dulla Makabila na Mfalme wa taarabu Mzee Yusuf waliteka

umati uliofurika katika kiwanja cha Nangwanda Sijaona.

Akifungua mashindano hayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amepongeza ubunifu wa waandaji wa mashindano ya mwaka huu kwa kuwashirikisha wasanii ili kuja kutoa burudani katika kipindi cha mashindano haya na kuonesha vipaji na vipawa walivyopewa na Mwenyezi Mungu.

Aidha, wakati wa ufungaji wa mashindano ya UMITASHUMTA wasanii wa kundi la Mr. Bluu na Msaga Sumu na vikundi vya kwaya na ngoma za asili kutoka mikoa mbalimbali vilipanda jukwani na kutoa burudani mwanana.

Pia, wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya, wakiongozwa na

Maua Sama na Chegge Chigunda wamekonga nyoyo za wanamichezo wa UMISSETA na kuleta hamasa kubwa kwa wanamichezo na wadau mbalimbali wa mkoa wa Mtwara walipotumbuiza jukwaani Juni 21, 2021 kwenye ufunguzi wa Mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi, amesisitiza kuwa mashindano haya yataendelea kutumbuizwa na wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya Mkoa wa

Mtwara, ambapo burudani pia kutoka vikundi vya ngoma za asili, kwaya na Sanaa nyingine vitaendelea kuonesha umahiri wao.



## Bilion 1.5 zatengwa kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya Utamaduni na Sanaa

Na Richard Mwamakafu, **MWANZA**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa amesema katika Bajeti Kuu ya Serikali takriban Shilingi Bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa.

Mhe. Bashungwa amesema hayo Juni 14, 2021 Jijini Mwanza katika ziara ya Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kukagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo ameeleza kuwa wizara hiyo kwa kushirikiana Wizara ya Fedha na Mipango

zinaendelea na utaratibu wa kurudisha Bahati Nasibu ya Taifa ili ya mapato yaende kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo.

Ametumia nafasi hiyo pia kumshukuru Mhe. Rais kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye nyasi bandia nchini ili miundombinu ya michezo iweze kupendeza na kuwa katika hali nzuri ambapo kwa kuanza italenga viwanja vya majiji na kadiri fedha itakavyopatikana viwanja vya kwenye Manispaa na Halmashauri vitafikiwa.

Aidha, Mhe. Bashungwa ametumia nafasi hiyo kuwapongeza Wasanii nchini pamoja na Wanahabari kwa kazi nzuri wanazofanya kwa maslahi ya Taifa ambapo amewataka kuendelea kumuunga mkono Mhe. Rais katika kuleta maendeleo endelevu nchini.



## Bunge lapitisha takriban sh. bilioni 54 kwa Wizara ya Habari

Na Eleuteri Mangi, Dodoma

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha na kuidhinisha Bajeti ya Wizara Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo jumla ya Sh. Bilioni 54 741,802,000 ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika fedha hizo, Sh. 19,146,653,000 zimepangwa kutumika kwa ajili ya mishahara, kiasi cha Sh. 14,880,149,000 matumizi mengineyo na kiasi cha Sh. 20,715,000,000 zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Bajeti hiyo imepitishwa Mei 31, 2021 Jijini Dodoma baada ya kuwasilishwa na Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo Mhe. Innocent Bashungwa na kujadiliwa na Wabunge kwa mujibu wa ratiba ya Bunge.

Kwa upande miradi ya maendeleo, Mhe. Bashungwa amebainisha kuwa Wizara itatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Ujenzi wa Chuo cha

Maendeleo ya Michezo Malya, ujenzi wa eneo Changamani la Michezo Dodoma, ujenzi wa eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam, ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzika wananchi na ukarabati wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.

Miradi mingine ni ukarabati wa Chuo Maendeleo ya Michezo Malya, Upanuzi wa Usikivu TBC, kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji pamoja na Mradi wa Elimu kwa Umma.



## Wizara ya Habari yavuka lengo ukusanyaji mapato mwaka 2020/2021

Na Eleuteri Mangi, **DODOMA**

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imevuka lengo la ukusanyaji mapato kwa kukusanya jumla ya kiasi cha Sh.1, 080,109,491 ambazo ni sawa na asilimia 113 hadi kufikia Mei, 2021 kutoka Sh. 960,000,000/= kiasi ambacho kilikadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2020/21.

Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo, Mhe. Innocent Bashungwa amesema hayo Mei 31, 2021 Bungeni Jijini Dodoma alipokuwa akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2021/2022.

Katika Sekta ya Utamaduni, Wizara

imeanzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ambao ulisajiliwa Septemba 30, 2020 kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa kazi za kiutamaduni na Sanaa katika mitaji na kuwajengea uwezo wa kitaalamu ili kuwawezesha kuandaa bidhaa bora zinazomudu ushindani kitaifa na kimataifa.



## Serikali kuondoa VAT kwenye nyasi bandia

Na Eleuteri Mangi, Dodoma

Serikali imependekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye Nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vya mpira vilivyopo kwenye Miji.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Nchemba Juni 10, 2021 Bungeni Jijini Dodoma alipokuwa anawasilisha Bajeti Kuu ya Serikali ambapo amesema kuwa msamaha huo utahusisha ridhaa kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF).

“Serikali imekubali kuongeza tozo katika Sports Betting kutoka asilimia 25 hadi 30 ya mapato ya sasa ili asilimia tano iliyoongezeka iende moja kwa moja katika Mfuko wa Maendeleo ya Michezo” amesema Dkt. Mwigulu.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa ameshukuru maamuzi hayo ya Serikali ambayo yanaenda kuendeleza sekta ya michezo nchini.

“Nimefurahi Bajeti ya mwaka huu imependekeza mapato ya michezo ya kubahatisha yachangie Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, pia kurejeshwa kwa Bahati Nasibu ya Taifa ambayo itachangia Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni” amesema Mhe. Bashungwa.





## Serikali yampongeza Diamond Platnumz

Na Freddy Mwakikato, DODOMA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa amempongeza Msanii Nasib Abdul (Diamond Platnumz) kwa kutajwa kuwania tuzo za heshima kipengele cha Wasanii waliofanaya vizuri Kimataifa zilizotangazwa hivi karibuni na Black Entertainment Television (BET) kwa mwaka 2021.

Mhe. Bashungwa ametoa pongezi hizo alipokuwa akijibu hoja ya Mhe. Stanslaus Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki Mei 31, 2021 ya

kutaka wananchi wahamasishwe ili kumpigia kura kwa wingi msanii huyo kwa kuteuliwa kugombea tuzo za BET kwa kuwa ameitangaza nchi kote ulimwenguni.

Ili kufanikisha msanii Diamond Platnumz kupata tuzo hiyo, Mhe. Bashungwa amesema Wizara kupitia BASATA inawahimiza Wabunge, Watanzania pamoja na wadau wengine ndani na nje ya nchi kumpiga kura kwa wingi kupitia link ya <https://www.bet.com/-awards/nom->

inees ili msanii huyo ashinde tuzo hiyo ambapo washindi watatangazwa Juni 27, 2021.

Diamond Platnumz ni msanii pekee kutoka Afrika Mashariki aliyeingia katika orodha ya Wasanii wanaowania tuzo hiyo duniani. Wasanii wengine ni Burna Boy na Wizkid kutoka Nigeria, Aya Nakamura na Youssoupha kutoka Ufaransa, Headie One na Young T & Bugsey kutoka Uingereza pamoja na Emicida wa Brazil.

# KONA YA KISWAHILI

Sasisha - Update

Tarakilishi - Computer

Kimemeshi - charger

kitumi - device

maunzi laini - software

maunzi ngumu - Hardware

kizinza - display

kichakata maneno - wordprocessor

sakinisha - install

wavuti wa walimwengu - World wide web (WWW)

pakua - download

chakata - process

vinjari - browser

nui - mode

kikusa - interface

programu tumizi - application

# MAMBO MAKUBWA AMBAYO WIZARA ITAYATEKELEZA KATIKA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/22

1. Kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari,
2. Kufunga mitambo ya masafa ya FM ya TBC katika mikoa ya Njombe, Songwe na Simiyu na Wilaya za Kilwa na Serengeti pamoja na kupanua usikivu wa redio katika maeneo ya Unguja na Pemba,
3. Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje Jijini Dodoma na kuimarisha Chaneli ya Tanzania Safari.
4. Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) itanunua mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji na kuwekeza zaidi kwenye habari mtandao.
5. Kuimarisha Muundo wa TCRA ili kusimamia utangazaji.
6. VKuhuisha na kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Utamaduni ya mwaka 1997 pamoja na kuchapisha na kusambaza kitabu cha Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Taifa,
7. Kuratibu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika iliyoasisiwa na azimio la Umoja wa Afrika mwaka 2011,
8. Kuendeleza mikakati ya kukitangaza na kubidhaisha Kiswahili
9. Kujenga jengo la kisasa la Ofisi za Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa Jijini Dodoma zitakazotumiwa na taasisi za BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania, COSOTA na BAKITA ili kuanza kuwawezesha wasanii kimitaji na mafunzo kwa wadau wa mfuko huo ambao umetengewa kiasi cha Sh.1, 500,000,000,
10. Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) litaimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaopanua wigo kwa kuwafikia wadau wa maeneo yote ya nchi wanaohitaji kupata huduma za usajili na vibali,
11. Baraza litatoa vitambulisho kwa wasanii kuwarahisishia kupata huduma mbalimbali ikiwemo Bima ya afya na huduma za kifedha kwa kuwa vitambulisho hivyo vitaunganishwa na mifumo ya taasisi zingine,

# MAMBO MAKUBWA AMBAYO WIZARA ITAYATEKELEZA KATIKA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/22

- 12.** Kuweka mfumo wa kisheria ya Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) utakaozweza kutozwa kwa tozo ya Blank Tape Remuneration/Levy pamoja na mfumo wa kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa hususan muziki na filamu katika vyombo vya habari na kukamilisha mfumo wa kielekroniki (online platform) kwa ajili ya kusambaza kazi za wasanii,
- 13.** Kuanzisha Tamasha Maalum la Michezo ya wanawake ili kuimarisha ushiriki wa wao katika michezo na kuibua vipaji vyao pamoja na kuzindua Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Michezo na kusimamia utekelezaji wake,
- 14.** Kuendelea kushirikiana na OR TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kusimamia shule maalumu za michezo zitakazotengwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kusimamia ufundishwaji wa somo la michezo kwenye shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na tahsusi zenye somo la michezo ili kukuza taaluma hiyo nchini,
- 15.** Kuratibu michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na kuratibu Siku Maalumu ya Michezo Kitaifa ili kuhamasisha michezo kwa jamii,
- 16.** Kufanya maboresho na kupanua Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ili kufanya chuo cha michezo cha kimataifa (sports academy).

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU**

**Wizara ya Habari, Utamaduni,  
Sanaa na Michezo**